East African Journal of Swahili Studies, Volume 7, Issue 1, 2024
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1959

East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 7, Issue 1, 2024
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Uamili wa Ufokasi katika Kudhihirisha Itikadi

*Dinah Sungu Osango*[1*] *Prof. Mwenda Mbatiah, PhD na Prof. Timammy Rayya, PhD*[2]

[1] Chuo Kikuu cha Nairobi, S. L. P. 30197 – 00100, Nairobi - Kenya.
[*] ORCID ID: https://orcid.org/0009-0001-5489-5466; Barua pepe ya mawasiliano: osangodinah72@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1959**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*28 Mei 2024*

**Istilahi Muhimu**:

*Ufokasi, Ngazi Ya Itikadi, Mkabala, Naratolojia, Itikadi Ya Kibepari, Imani.*

## IKISIRI

Makala haya yanachunguza ngazi ya itikadi na uamilifu wake katika riwaya teule za Kiswahili kupitia kwa ufokasi. Riwaya teule ni Haini (Adam Shafi, 2003), Makuadi wa Soko Huria (C. Chachage, 2005), Harufu ya Mapera (K. Wamitila, 2012), Hujafa Hujaumbika (F. Kagwa, 2018), Ndoto ya Almasi (Ken Walibora, 2006) na Nyuso za Mwanamke (S. Mohamed, 2010). Ngazi ya itikadi ni mojawapo ya ngazi mbalimbali za ufokasi zilizopendekezwa na wananaratolojia. Kimsingi, ufokasi ni mkabala ambao huchukuliwa katika kuwasilisha simulizi na kuikuza hadithi kwa ujumla. Data ya kuudhibiti na kuthibitisha madai ya mjadala wetu imetolewa katika riwaya teule. Uteuzi wa riwaya hizi unahalalishwa kwa misingi kwamba, hizi ni riwaya zilizo na matini pana zinazowezesha udondoaji wa mifano faafu inayodhihirisha ngazi ya itikadi na wakati huo huo kudhihirisha uamili wa ngazi hiyo katika simulizi. Mjadala wa kimsingi katika makala haya umekitwa na kuongozwa na teneti za kimsingi za nadharia ya naratolojia ambayo inatambua ufokasi kama kipengele muhimu katika uwasilishaji wa simulizi. Uchunguzi wetu umeonyesha kuwa, kupitia kwa ufokasi nje na ndani, waandishi wa riwaya teule wamedhihirisha ngazi ya itikadi. Imebainika kuwa wahusika mbalimbali huwa na tabia, mitazamo, misimamo na hisia fulani kuhusu masuala mbalimbali kutokana na athari za itikadi zinazotawala mazingira au matamanio yao.

**APA CITATION**

Osango, D. S., Mbatiah, M. & Rayya, T. (2024). Uamili wa Ufokasi katika Kudhihirisha Itikadi. *East African Journal of Swahili Studies, 7*(1), 272-282. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1959.

**CHICAGO CITATION**

Osango, Dinah Sungu, Mwenda Mbatiah and Timammy Rayya. 2024. "Uamili wa Ufokasi katika Kudhihirisha Itikadi". *East African Journal of Swahili Studies* 7 (1), 272-282. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1959.

**HARVARD CITATION**

Osango, D. S., Mbatiah, M. & Rayya, T. (2024) "Uamili wa Ufokasi katika Kudhihirisha Itikadi", *East African Journal of Swahili Studies*, 7(1), pp. 272-282. doi: 10.37284/jammk.7.1.1959

**IEEE CITATION**

D. S. Osango, M. Mbatiah & T. Rayya "Uamili wa Ufokasi katika Kudhihirisha Itikadi", *EAJSS*, vol. 7, no. 1, pp. 272-282, May. 2024.

**MLA CITATION**

Osango, Dinah Sungu, Mwenda Mbatiah & Timammy Rayya. "Uamili wa Ufokasi katika Kudhihirisha Itikadi". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 7, no. 1, May. 2024, pp. 272-282, doi:10.37284/jammk.7.1.1959.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1959

## UTANGULIZI

Uchunguzi wetu umedhamiria kuonyesha jinsi ufokasi unadhihirisha ngazi ya itikadi katika riwaya teule. Ngazi ya itikadi inahusisha uchunguzi wa imani, turathi na kaida za jamii husika zinavyodhihirishwa na wahusika mbalimbali kupitia kwa ufokasi ndani na ufokasi nje. Itikadi ina misingi yake katika mawazo ya Marx na Engels (1977) wanaposema kuwa itikadi ni dhana na imani za tabaka tawala katika kipindi maalum. Kulingana nao, dhana na imani za tabaka tawala ndizo hutamalaki taratibu za kuunda fikra, mawazo na mielekeo ya wanajamii kwa ujumla. Wanaendelea kusema kuwa, itikadi hujumuisha fikra zote na maoni ya wanadamu kuhusu yale wanayoyasema na jinsi wanavyofikiria kuhusu siasa, sheria, maadili, dini na falsafa.

Althusser (1981) anaunga mkono mawazo haya ya Marx na Engels anaposema kuwa itikadi huendelezwa kwa umoja wa wanajamii ambapo nguvu na mamlaka hutumiwa ili kudhibiti hali ya kiutawala. Kinachotumiwa katika kuuendeleza utawala ni vyombo vya dola kama vile polisi, jeshi, mahakama, na magereza. Kando na vyombo vya dola, kuna vyombo vingine kama vile: kanisa, shule, vyombo vya habari, siasa, familia, sheria, vyama vya wafanyakazi na utamaduni ambavyo pia hutumiwa kuendeleza itikadi ya tabaka tawala. Vyombo hivi hufanya kazi kwa njia huru kiasi bila kuwa na lengo la moja kwa moja la kudhibiti na kutawala. Kwa hivyo, ni kawaida kushuhudia mifumo ya kiutawala kama ile ya kikabila, kirangi na hata ile ya kuumeni ikiendelezwa bila pingamizi. Hali hizi huchukuliwa kwamba ni za kawaida hivyo basi wanaonyanyaswa huenda hata wasijue wananyanyaswa.

Mitazamo, turathi na imani za binadamu huchangia pakubwa katika mahusiano ya watu katika jamii. Kutokana na mahusiano hayo, aina mbalimbali za itikadi huibuka. Gramsci (1985) anasema kuwa itikadi hutokana na ukawaida na ukubalifu ambapo watu huzoea hali fulani na kuichukulia hali hiyo kuwa ya kawaida. Hata hivyo, baadhi baadhi yazo huwafanya watu kuwa na mivutano au migogoro. Mivutano hii husababisha kuwepo kwa mabadiliko ya aina fulani. Mojawapo ya mabadiliko hayo hutokea kutokana na mapambano ya kitabaka ambapo jamii yoyote ile huendeshwa na nguvu za kiuchumi (Marx, 1979). Eagleton (1976) anahusisha itikadi na fasihi anaposema kuwa itikadi ni fikra, amali na hisia ambazo mwanadamu hupitia katika jamii yake kwa kipindi maalum na huweza kupatikana tu kupitia fasihi. Kulingana naye, kuelewa itikadi ni sawa na kuelewa historia ya yaliyopita huku yale mambo ya sasa yakichunguzwa kwa undani ili kuibua uzunduzi wa kujikomboa. Mohamed (1995) anaunga mkono mawazo ya Eagleton anaposema kuwa itikadi ni muhimu katika kazi za fasihi kwani ndiyo humwongoza mtunzi kuteua yale atakayowasilisha katika simulizi yake. Katika utafiti huu, tutachunguza kaida zinazohusishwa na imani, turathi, amali na mitazamo ya kibinafsi na ile ya kilimwengu kuhusu masuala mbalimbali kama yanavyodhihirishwa na wahusika mbalimbali katika riwaya teule, kupitia kwa ufokasi.

### Msingi Wa Nadharia

Makala haya yanaongozwa na nadharia ya naratolojia. Nadharia ya naratolojia ina misingi yake katika kipindi cha urasimi ambapo Plato na Aristotle walichangia katika kukuza nadharia ya simulizi (Gholami, 2013). Makala ya kwanza ambayo yanarejelea nadharia ya simulizi ni yale ya Plato katika kitabu chake cha *The Republic*. Katika kazi hiyo, Plato anaelezea istilahi mbili za kimsingi kuhusiana na usimulizi; dhana ya mimesia kwa maana kuwa, hadithi inasimuliwa moja kwa moja mbele ya hadhira; na dhana ya daijesia ambapo msimulizi hupewa jukumu la kusimulia matukio ya hadithi. Aristotle naye anafafanua nadharia hii ya naratolojia katika *Poetics* anapoelezea maana ya tanzia. Anasema kuwa, ploti ya tanzia lazima iwe na mwanzo, kilele, na mwisho. Maelezo yake kuhusu tanzia katika ushairi yalikuwa na mchango mkubwa katika kwa uelewa wa dhana ya naratolojia.

Kuibuka kwa hadithi fupi na riwaya kama tanzu za fasihi katika karne ya 18 kulishurutisha wananadharia wa baadaye kuanza kuiangalia upya na kutathmini nadharia ya simulizi.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Nadharia ya simulizi haikuwa na budi kufanyiwa marekebisho na mabadiliko ya kimsingi yaliyofikia kuibuka kwa nadharia ya naratolojia kama inavyoeleweka sasa. Wananaratolojia kama vile Roland Barthes (1966) Tzvetan Todorov (1968) na Algirdas Greimas (1973) waliamini kuwa palikuwa na haja ya kutunga sheria ambazo zingedhibiti simulizi ili kufanikisha uainishaji wa simulizi mbalimbali kwa kadri zilivyojitokeza katika riwaya, hadithi fupi, na bunilizi nyinginezo zilizokuwa na wasifu wa usimulizi. Wananaratolojia hawa wanaweza kuangaliwa kuwa ndio waliokuwa wa kwanza kuhusisha simulizi za kinahari katika hadithi na nadharia hii.

Kikundi kingine cha wananaratolojia kama vile Vladimir Propp (1968), Gérard Genette (1972) na Seymour Chatman (1978) kilifuata mtazamo wa kuchambua simulizi kwa kurejelea diskosi. Wananadharia hawa walijishughulisha kutunga sheria ambazo walizichukulia kuwa faafu kudhibiti simulizi katika riwaya kinyume na ilivyokuwa hapo awali. Kwa mfano, Genette (1972) alichangia katika ukuzaji na uimarishaji wa nadharia ya naratolojia, hasa inapozingatiwa kwamba, Genette anatambulisha mambo matatu muhimu yanayoshurutisha kuzingatiwa katika simulizi. Kimsingi, mambo haya—yaani simulizi, hadithi na usimulizi ni uhalisia unaotegemeana, unaojengana na kujalizana. Kwa sababu ya kujibainisha kwa misingi iliyo na mahusiano ya karibu sana, Genette anapendekeza kutofautishwa kwa anayesimulia na anayeona matukio yanayosimuliwa katika simulizi. Kwa hivyo, anapendekeza istilahi ufokasi kama kipengele kinachomdhihirisha anayeona matukio na anayesimulia matukio.

Mbali na haya, Genette anatambua aina tatu za ufokasi: ufokasi ndani, ufokasi nje na ufokasi nunge. Kuibuka kwa istilahi na dhana nzima ya ufokasi, kuliwachochea wananaratolojia wengine kufanya utafiti zaidi ili kutatua utata uliokuwepo hapo awali kuhusu tofauti kati ya anayesimulia hadithi na yule anayeona matukio. Kwa mfano, Rimmon-Kenan (1983) na Bal (1985) walichangia katika kuikuza istilahi hii huku wakipendekeza miundo mbalimbali ya kufanikisha uchambuzi wa matini za kibunilizi. Hivyo basi, nadharia ya naratolojia inatuwezesha kuchunguza ngazi ya itikadi ambayo ni mojawapo ya ngazi mbalimbali za ufokasi. Uchunguzi wetu unajikita katika kuonyesha jinsi ufokasi unadhihirisha itikadi ya kibepari katika riwaya teule.

## MBINU ZA UTAFITI

Uchunguzi wetu umetumia mbinu ya utafiti stahilifu. Hii ni mbinu ambayo hukuza maelezo ya matukio ya kijamii (Hancock, 2002). Mbinu hii imetufaa kwa kuwa uchunguzi wetu unahusu matini simulizi. Uteuzi wetu wa data ulitegemea vipengele vya ngazi ya itikadi vinazojitokeza katika riwaya teule. Licha ya kuwa kuna riwaya nyingi za Kiswahili ambazo zinazodhihirisha ngazi ya itikadi, tumejikita tu katika riwaya sita. Riwaya hizo ni *Haini* (Adam Shafi, 2002), *Makuadi wa Soko Huria* (C. Chachage, 2005), *Harufu ya Mapera* (K. Wamitila, 2012), *Hujafa Hujaumbika* (F. Kagwa, 2018), *Ndoto ya Almasi* (Ken Walibora, 2006) na *Nyuso za Mwanamke* (S. Mohamed, 2010). Uchunguzi wetu umekuwa wa maktabani ambapo tumezisoma riwaya teule, vitabu na makala mbalimbali ambayo yametufaa katika kuukuza mjadala wetu.

### Matokeo ya Uchunguzi

Uchunguzi wetu umedhihirisha kuwa waandishi wa riwaya teule wametumia ufokasi nje na ndani ili kudhihirisha ngazi ya itikadi. Imedhihirika kuwa, kaida zinazohusishwa na imani, turati, amali na mitazamo ya kibinafsi na ile ya kilimwengu kuhusu masuala mbalimbali imedhihirishwa na wahusika mbalimbali katika riwaya teule, kupitia kwa ufokasi. Uchunguzi wetu umejikita katika itikadi ya kibepari.

### Itikadi ya Kibepari

Ubepari ni mfumo wa kiuchumi, kisiasa na kijamii wa umiliki wa mali, biashara na viwanda kwa lengo la kutengeneza faida kubwa iwezekanavyo kwa kampuni na watu wenye kufanikiwa (Kennedy, 1978). Ubepari hufanikisha umiliki wa njia kuu za kiuchumi

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1959

ambapo biashara, viwanda na vitega uchumi vingine vinatawaliwa na watu binafsi kwa kiasi kikubwa. Katika mfumo huu ni watu wachache tu wanaomiliki nyenzo za uzalishaji huku wengi wakisalia maskini ambao hunyanyaswa na matajiri. Wanaoamini katika mfumo huu huwa wanaendeleza itikadi ya kibepari. Itikadi hii imedhihirika katika riwaya teule kupitia kwa ufokasi ndani na nje, ambapo wahusika wanaoamini katika itikadi hii wanaendeleza mfumo wa kibepari. Itikadi hii hudhihirika kupitia kwa ukandamizaji ambapo vyombo mbalimbali kama vile mfumo wa kiuchumi, asasi za utawala, elimu, utamaduni, ndoa na mapenzi, mfumo wa kuumeni, na dini hutumiwa ili kufanikisha ubepari. Itikadi ya kipebari inajitokeza katika riwaya tulizoziteua kupitia kwa wafokasi mbalimbali. Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*, Bwana Hila anawakilisha watu wachache wanaomiliki mali nyingi huku wakiwanyanyasa maskini, kwa kuwa anaongozwa na itikadi ya kibepari. Hila alikuwa tajiri mkubwa aliyemiliki mashamba mengi na majumba ya kifahari. Kupitia pia kwa kipengele cha lugha ambapo mwandishi amempa jina Hila ambalo ni jina la kimajazi, mhusika huyu anaendeleza hila zake anapowanyang'anya majirani wake mashamba yao. Hali hii inadhihirika kupitia kwa msimulizi-mfokasi ambaye ni mwanawe, msomaji anajulishwa jinsi umiliki wa mali yake haukuwa halali. Kwa mfano, anasema:

> *Bado mpaka leo wakulima wananung'unika, na hawatasita milele ingawa hawajui wamlalamikie nani. Vipi yule mfua-vyoo jana leo na awe tajiri mkubwa kiasi hiki? Wao walikuwa wapi alipojitutumua? Hakusomba mali tu, bali kaiba heshima ya wakulima baada ya kuwanyang'anya ardhi na uhuru wao… Ghafla amepata nguvu zinazomsimamisha kumsuta kila mtu... (uk. 37).*

Bwana Hila anasemekana kuanza kuchukua mashamba ya wakulima hao kidogo kidogo kwa malipo madogo kisha baadaye akawasukuma pembezoni kwa mkono wa kuvuruga sheria. Hili lilikuwa kinyume na matarajio ya wananchi wenzake hasa baada ya kupigania haki na usawa, walipomwondoa mkoloni. Jambo hili linaibua mgogoro wa kitabaka ambapo wahusika wanadhihirisha mitazamo tofauti. Bwana Hila anachukua mtazamo wa kikoloni wa kuhifadhi mali nyingi huku akiwatumia watu wa tabaka la chini kumhudumia kwa malipo duni, ilhali mwenyewe na watu wa tabaka la juu wakistarehe kwa jasho la maskini. Kwa upande mwingine, maskini wanaiona hali hii kama unyanyasaji kwa kuwa inaenda kinyume na lengo lililokuwepo wakati wa kumwondoa mkoloni.

Hali hii haikumfurahisha mwanawe, Nana, ambaye anaenda kinyume na mtazamo wa babake. Kupitia kwa ufokasi ndani, anadhihirisha chuki yake dhidi ya tabia ya babake anaposema kuwa kila siku moyo wake ulipiga fundo alipokumbuka jinsi pesa zilivyofujwa ovyo na jinsi watu wengine ambao hawakuwa kama wao walizama katika tope za ufukara. Wengi hasa vijana hawakuwa na kazi wala bazi (uk. 31-32). Uamuzi wake wa kuupinga msimamo wa babake unaibua mgogoro baina yao. Mgogoro huu unamfanya Nana kutoroka nyumbani kwao na kuhamia katika mtaa wa mabanda anakojitafutia riziki yake. Baadaye, anafanikiwa maishani baada ya kuanza biashara yake binafsi. Aidha, inadhihirika kuwa, kutokana na tofauti za kiuchumi, matajiri hawatangamani na maskini. Kwa mfano, Bwana Hila hatangamani na majirani zake kwa kuwa walikuwa maskini. Anapoandaa sherehe nyumbani kwake, anawaalika watu wa tabaka la juu pekee. Nao maskini wanasalia wakinusia tu harufu ya chakula kilichopikwa kwa wingi katika sherehe hizo. Hili linadhihirika kupitia kwa ufokasi ndani Nana anaposema kuwa siku walizokuwa na sherehe, hakuna mchochole hata mmoja aliyealikwa katika sherehe hizo. Siku ya sherehe, maskini walisikia tu sauti na vicheko vya satarehe zilizokuwa zikiendelea. Kwa mfano, anasema:

> *... Hakuna mchochole aliyealikwa katika sherehe hizo…* (uk. 31).
>
> *... Au siku kama ya leo, mivumo ya sauti na vicheko vya starehe vinapochupa makuta na kukata hewa kwenda kuwajeja wao*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1959

> *hohehahe… Au harufu za vyakula zinapowapenya puani huko waliko, kuwafanya walambatie mate na kutambua kwamba kwa Bwana Hila (huyu babangu) leo kuna mambo* (uk. 37).

Dondoo hili linadhihirisha hisia za Nana kuhusu suala zima la utabaka ambao huibuliwa kutokana na itikadi za kipebari. Kulingana naye, hali hii hafai na ndiyo sababu alizipinga sherehe za babake zizolinuia kuwafurahisha tu watu wa tabaka la juu.

Uchunguzi wetu umebaini kuwa, wahusika wanaoamini itikadi ya kipebari, ubebari huwa mbioni kuhakikisha kuwa wanamiliki nyenzo kuu za uzalishaji mali. Ubepari hufanikisha kundi moja, ambalo huwa tabaka la juu kumiliki mfumo wa uzalishaji mali huku tabaka la chini likimiliki nguvu na uwezo wa kufanya kazi. Kwa kuwa nyenzo za uzalishaji mali ni chache, ni watu wachache wenye uwezo wa kuimiliki. Hivyo basi, idadi ya matajiri inakuwa ndogo sana ikilinganishwa na maskini ambao huwa wengi sana.

Hali kama hii pia inadhihirika katika *Ndoto ya Almasi* wakati msimulizi-mfokasi anaposema kuwa nchi ya Kenya ina mamilionea kumi na wachochole milioni kumi (uk 9). Licha ya msemo huu kusemwa katika miaka ya sabini, jambo hili bado linaendelea kudhihirika katika nchi hii hadi sasa. Kwa mfano, matajiri wachache kama vile babake Japheth wanamiliki mashamba maddal basari katika eneo la Kitale. Licha ya kumiliki mashamba haya, tajiri huyu bado ana tamaa ya pesa zilizotengewa misaada ya wanafunzi maskini. Anatumia njia za kifisadi ili kumwandikisha mwanawe kuwa mmoja wa wale wanaopata ufadhili wa watoto maskini. Tabia hii inadhihirisha tamaa na ubinafsi alionao mhusika huyu - wa kutaka kuendelea kuwa na mali nyingi huku maskini kama vile Almasi wakikosa pesa za msaada (uk. 35).

Katika *Harufu ya Mapera*, wahusika kama vile Pipo Kenya wanadhihirisha itikadi ya kibepari kwa kuwa yeye na wenzake wachache wanamiliki mali nyingi huku wananchi wengi wakikosa makaazi. Kwa mfano, anamiliki mashamba makubwa huko vijijini, majumba mengi mjini Nairobi na biashara mbalimbali katika sehemu mbalimbali ulimwenguni. Hata hivyo, sehemu kubwa ya mali hiyo aliipata kwa njia zisizo halali. Pipo anatumia nafasi yake kisiasa ili kujilimbikizia mali hiyo huku sheria ikifinyangwa ili kumlinda. Sawa na matajiri wengi ambao huwadhulumu maskini ili kupata mali yao, Pipo anamuua babake Matata na kumnyang'anya stakabadhi za shamba lake ambazo anazitumia kuubadilisha umiliki wa shamba lake. Pia, kutokana na nafasi yake ya kisiasa, anafanikiwa kufanya biashara ya magendo inayomfanikisha kuwa tajiri zaidi. Kwa mfano, anawasiliana na rafiki yake jinsi ya kufanikisha biashara bila ya kupata hasara. Rafiki yake Gopal anamshauri aongeze bei ya viatu kwa asilimia mia moja kisha aipunguze bei hiyo kwa asilimia hamsini au sitini. Akishafanya hivyo, alifaa kuandika "GRAND SALE" kisha atangaze kwenye vyombo vya habari kama vile magazeti (uk. 244).

Pipo anatumia mbinu za kijanja kama hizi ili kupata faida maradufu kutoka kwa wananchi wasioufahamu mtego huo. Baada ya Pipo kupokea matokeo mazuri, anakuwa na kiburi na kushangaa jinsi wananchi walivyo wajinga sana, kwani wanaingia katika mtego wake haraka bila kuushuku. Hali hii inadhihirika kupitia kwa ufokasi ndani anaposema, ".... "Watu wa Nairobi Gopal ni mabwege wakubwa!" (uk. 245). Hatimaye, huu ujanja wake ukawa nguzo muhimu ya kuyabadilisha maisha yake kiuchumi. Aidha, anakuwa mstari wa mbele kuwatetea marafiki zake waliokuwa wakiuza bidhaa ambazo zimeharibika, huku wakibadilisha tarehe kwenye vibandiko ili kuepuka mkono wa sheria. Kimsingi, Pipo na matajiri wenzake wako mbioni kujinyakulia mali nyingi kwa kuwa wanaongozwa na itikadi ya kibepari. Hali hii inadhihirisha sifa zao za kuwa binafsi na wenye tamaa.

Itikadi ya ubepari pia inajitokeza katika *Makuadi wa Soko Huria* kupitia kwa ufokasi ndani wakati ambapo Wazungu kadhaa wanajadiliana jinsi ya kuendelea kumiliki njia za uzalishaji mali katika nchi za Afrika. Licha ya kuwa nchi husika imepata

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1959

uhuru, bado kuna wale Wazungu kama wanavyojulikana na wenyeji kama 'makuadi' ambao wako mbioni kumiliki nyenzo kuu za kuzalisha mali. Kwa mfano, baada ya Bwana Mooney na wenzake kuwekeza katika miradi mbalimbali nchini Tanzania, wanataka sasa kuwekeza katika uuzaji wa bunduki, ili pia nao wapate ulinzi wa miradi yao kama inavyodhihirika katika dondoo hili:

> *"… Kwa ajili ya huu mradi wangu mmoja tu, ninahitaji silaha kwa ajili ya walinzi si chini ya mia mbili. Kadhalika, nilikutana na baadhi ya wawekezaji ambao wako kwenye sekta za madini na misitu ambao wanalalamika kuhusu tatizo hilohilo… Lakini sisi tunahitaji kuwa na majeshi ya ulinzi yetu wenyewe."* (uk. 122).

Licha ya kuwa wananuia kuagiza silaha kwa lengo la kuilinda miradi yao, lengo lao kuu ni kuiendeleza biashara hii kisiri bila ya wao kujulikana. Hii ndiyo sababu mara kwa mara kuna vita vya wenyewe kwa wenyewe katika mataifa ya Barani Afrika kwa kuwa silaha zinazoagizwa kwa njia kama hii ndizo hutumika katika vita hivyo. Kwa hivyo, wafanyabiashara wa silaha hizi huchochea vita ambapo lengo lao huwa kupata soko la kuuza silaha zao.

Katika jamii ya kimwinyi watu hagawika katika matabaka kutokana na kutokuwepo kwa usawa wa kiuchumi miongoni mwa watu. Kundi moja ambalo huwa tabaka la juu humiliki mfumo wa uzalishaji mali huku tabaka la chini likimiliki nguvu za kuzalisha mali. Hali hii husababisha kuwepo kwa tofauti za kiuchumi, kijamii na hata kisiasa. Kulingana na Marx (1979), matabaka huwa na mikinzano kwa sababu jamii daima iko katika harakati za kufanya hali zao kuwa bora zaidi.

Aidha, Itikadi ya kibepari huwawezesha watu wa tabaka la juu kupokea huduma nyingi bila shida yoyote kutokana na uwezo wao wa kiuchumi. Shivji (2002) analiita tabaka hili "tabaka la walala heri" kwa kuwa maisha yao huwa bora. Hali hii ni kinyume cha watu wa tabaka la chini ambao hudhalilishwa kutokana na nafasi zao za chini kiuchumi. Kinaya ni kuwa watu wengi wa tabaka la chini huchangia pakubwa katika kuiendeleza hali hii. Kwa mfano, katika *Hujafa Hujaumbika*, mhudumu katika hospitali ya Dharura Women's Hospital anawahudumia wagonjwa kulingana na hadhi yao ya kiuchumi. Anamdharau na kukataa kumhudumia Peusi wakati anapofikishwa kwenye hospitali hiyo, kwa kuwa alikuwa ameletwa hapo akiwa amebebwa kwenye rukwama. Kulingana naye, mtu yeyote anayesafirishwa kwa rukwama ni maskini. Kwa upande mwingine, mhudumu huyu anaonyesha furaha na kumkimbilia mgonjwa anayeletwa kwenye hospitali hiyo akiwa katika gari kubwa aina ya BMW. Baada ya kuwasili kwa mgonjwa huyo, muuguzi huyu anampa huduma ya kwanza mara moja kinyume na hali ilivyokuwa kwa Peusi. Lakini asichokifahamu ni kuwa, Peusi alikuwa mwana wa Bi. Timazi, ambaye alikuwa amelezwa kwenye hospitali hiyo baada ya kubakwa na majambazi waliokuwa wameivamia nyumba yao wakati Bi. Timazi alikuwa amesafiri.

Inasadifu kuwa Peusi alikuwa ameletwa hapo na Adili, mwendesha rukwama ambaye pia ndiye alikuwa amemleta Bi. Timazi katika gari lake kubwa. Mabadiliko ya tabia ya muuguzi anapomwona Bi. Timazi akiletwa hospitalini yanawashangaza sana Mwanga na Adili. Kupitia kwa ufokasi ndani, Adili anadhihirisha kuwa hii ni hali ya kawaida kwa binadamu anaposema, "Usijali. Hivi ndivyo walivyo walimwengu. Huabudu mali. Usimchukulie kwa uzito wowote. Si sisi tuliokuja akatutupia cheche za matusi? Tumebadilika vipi? Ukweli ni kuwa tulienda maskini tukarudi matajiri. Si neno, kwake mtu ni alicho nacho." (uk. 65).

Hali hii inatangaza itikadi ya muuguzi huyu kuhusu mali. Kwake, matajiri wanastahili kukwezwa kwa kupewa huduma bora. Muuguzi huyu anakuzwa kama kigeugeu ambaye anabadilisha huduma zake kulingana na tabaka analotoka mgonjwa. Kwa upande mwingine, Adili anadhihirishwa kuwa na utu kwa kuwa yuko tayari kuwasaidia watu wakiwa katika shida bila kuzingatia tabaka wala mazingira. Ni yeye pekee ndiye alikubali kumsaidia Mwanga alipokuwa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1959

njiani akiwa na dadake Peusi. Hii ni baada ya watu wengi wenye magari kukataa kumsaidia licha ya kuomba msaada wao.

Baadhi ya maskini katika tabaka la chini wana imani kuwa shida zao zote huwa zimesababishwa na watu kutoka katika tabaka la juu. Hali hii daima husababisha mikinzano kama alivyosema Marx (1979). Maskini hao huwajumuisha matajiri wote kuwa madhalimu. Hivyo basi, mara kwa mara wanawaelekezea matajiri wote hasira zao bila ya kubagua.

Hali hii inadhihirika katika *Harufu ya Mapera* wakati ambapo Jimna, kijana wa tajiri mmoja, anashambuliwa na waandamanaji waliokuwa wakipigania haki yao ya kunyakuliwa kwa mashamba yao. Kwa kuwa Jimna alijipata katikati ya maandamano hayo huku akiwa katika gari kubwa, anazomewa na kurushiwa mapera na wanaandamaji hao. Mmojawapo anadhihirisha pengo lililopo kati ya matabaka haya mawili anaposema, “Ndugu zako nani? Kuna udugu gani kati ya maskini na tajiri katika nchi hii? Unadhani sisi tunabugia mayai na kula viga vya kuku kila asubuhi? Unadhani tunafyonza maji ya tikitimaji kama nyie?” (uk. 30)

Hali kama hii inawafanya matajiri wengi kuhofia kuhusiana na maskini kutokana na hofu ya kushambuliwa wakati wowote. Hii ndiyo sababu wengi wao hutilia maanani suala la ulinzi huku wakiwaajiri walinzi wengi. Aidha, matajiri wengi wanachukulia watu wa tabaka la chini kuwa hatari, wezi, wachawi na wenye wivu. Hali hii inadhihirika kupitia kwa mawazo ya Isabelle anapokumbuka jinsi babake alivyokuwa amemwonya kuhusu watu wa mashambani kama ifuatavyo, “... Ni watu wanaoishi katika kipindi kingine na sisi. Waambae Isabelle wangu; wanachojua ni wivu na uchawi tu na wanatuonea wivu sasa kutokana na maendeleo yetu makubwa ...” (uk. 48). Maneno haya yanamfanya Isabelle kuwa na mtazamo hasi kwa wasichana aliokuwa amekutana nao katika shamba la babake. Alikuwa karibu kuwafyatulia risasi kwa tuhuma za wizi wa mapera.

Uchunguzi wetu pia umeonyesha kuwa, baadhi ya wahusika bado wanaendeleza utabaka kwa misingi ya rangi licha ya kuwa mataifa husika yamepata uhuru. Hili linadhihirika katika *Makuadi wa Soko Huria* wakati ambapo Msakapanofu anasimulia tafrija na mikutano iliyokuwa ikifanyika katika baadhi ya mitaa ya kifahari ambapo walioalikwa walikuwa Wazungu na Waafrika wachache sana, ambao walialikwa kwa malengo mahususi. Kwa mfano, mfokasi-mhusika anasema kuwa kulikuwa na sehemu fulani za starehe zilizokuwa zimeibuka tangu mwishoni mwa miaka ya themanini, zikiendeleza shughuli zake kama vilabu, lakini ambazo pia zilikuwa na masharti ambayo yaliruhusu uanachama kwa watu wa aina fulani tu. Sehemu hizo ziliendeleza ubaguzi wa rangi na nasaba.

Waafrika wachache walioalikwa katika klabu za aina hii, walikuwa ni mawaziri wa serikali, makatibu wakuu na wakurugenzi. Hawa walialikwa tu iwapo Wazungu hao walihitaji misaada kutoka kwao. Kwa mfano, Mheshimiwa Luhala alikuwa amealikwa katika mojawapo ya tafrija hizo, kwa kuwa Wazungu waliokuwa wamemwalika walitaka awe mstari wa mbele katika bunge kuipitisha sheria iliyowaruhusu wageni kumiliki mashamba makubwa nchini. Kwa hivyo, ni dhahiri kuwa wahusika katika tafrija hizi wanaunga mkono itikadi ya kitabaka ambayo haiwaruhusu watu kutangamana wapendavyo.

Utafiti umedhihirisha kuwa ndoa inatumiwa kama nyenzo ya kuendeleza itikadi ya kitabaka. Jamii inayotawaliwa na utabaka hushuhudia mikinzano mikubwa ya kindoa kwani inakumbwa na vikwazo vingi vya kimahusiano. Familia zinazotoka katika tabaka la juu haziwaruhusu wana wao kuwa na mahusiano na watoto kutoka katika tabaka la chini. Kwa mfano, katika *Harufu ya Mapera*, uhusiano kati ya Jude na msichana mmoja aliyetoka katika tabaka la chini haukudumu kwa kuwa babake aliukatiza uhusiano huo ghafla. Haya yanadhihirika kupitia kwa ufokasi nje wakati ambapo msimulizi-mfokasi anasimulia jinsi uhusiano huo ulisitishwa kupitia kwa analepsia:

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1959

> ... *Akakumbuka jinsi babake alivyotaka kummeza alipotambua uhusiano wao; nafuu huyo mamake alimwonea huruma kidogo. Jinsi msichana alivyovurumishwa, akayoyomea mbali asionekane tena… kwa kiasi fulani alihisi kama hisia zake za mapenzi alizokuwa nazo kwa msichana huyo zilifunikwa kwa utando mwepesi tu…* (uk. 379).

Uamuzi wa kumfukuza msichana huyo ulimwacha Jude na athari kubwa ya kisaikolojia, kwani licha ya kuhusiana na wanawake wengine wawili katika maisha yake ya baadaye, moyo wake haukuwahi kutulia kutokana na kumkosa mpenzi wake wa kwanza. Kwa upande mwingine, jamii kutoka katika tabaka la chini, hujitahidi kuvuka kutoka kwenye tabaka la chini hadi lile la juu kupitia kwa ndoa. Wengi wao hufanya hivi kwa lengo la kutaka kuziba pengo lililopo la kiuchumi kwa kupokea mahari na malipo mengine. Kwa mfano, katika *Nyuso za mwanamke*, babake Bimkubwa anamwoza bintiye kwa mwanamume aliyekuja kwake kumposa, kwa kuwa alikuwa na mali nyingi. Mzee huyu hakujali hisia za mwanawe kuhusu mwanamume huyu. Aliposikia kuwa mwanamume aliyekuja kumposa bintiye alikuwa ameleta dhahabu, almasi na lulu, aliamua kumwoza mwanawe bila kushauriana na mkewe. Mkewe alipojaribu kumuuliza sababu ya kufanya uamuzi wa haraka, alimwita mpumbavu kwa kukataa utajiri ule wa ajabu.

Babake Bi. Mkubwa aliongozwa na tamaa ya pesa ndiposa akaamua kumuoza bintiye bila kuihusisha familia yake katika mpango wake. Haya yanatokea licha ya kuwa mwanamume huyu alifahamu vyema kuwa bintiye alikuwa na mchumba mwingine ambaye walikuwa wamepanga kufunga ndoa. Juhudi za Bi. Mkubwa za kutorekea msituni baada ya kujulishwa kuhusu posa yake hazikufua dafu kwani babake aliwatuma watu wengi katika msitu huo ili kumkamata. Baadaye alilazimishiwa mume ambaye hakumpenda. Hivyo basi, mwanamke katika jamii hii hana uhuru na usemi kuhusu uteuzi wa mchumba, kwa kuwa uamuzi huo hufanywa na wanaume ambao mara nyingi huzingatia mali kama kigezo cha kuwachagua waume za mabinti zao.

Aidha, baadhi ya wahadhiri wanaendeleza itikadi ya kipebari wanapoendeleza utabaka katika vyuo vikuu wakati wanakubali kuhongwa ili kuwapa wanafunzi alama za bure. Wanaofaidika katika mpango huu, ni wanafunzi kutoka katika tabaka la juu kwani wao ndio wenye uwezo wa kutoa hongo. Kwa mfano, Jimna alikuwa na mazoea ya kutohudhuria masomo yake chuoni kwa kuwa alikuwa na mazoea ya kuwahonga wahadhiri, ambao baada ya kulipwa walimpa alama za bure (uk. 172). Kutokana na hali hii, vijana wengi kutoka katika tabaka la juu watafanikiwa kumaliza masomo yao kwa njia nyepesi, kisha kupata nafasi bora za kuajiriwa kwa kuwa elimu inatumiwa kama kigezo cha kuwaajiri watu. Hivyo basi, elimu inatumika kama asasi mojawapo inayotumiwa na watawala kuendeleza utawala wao kwa lengo la kuhifadhi tabaka lao kama alivyosema Althusser (1981).

## Sheria

Sheria hutumiwa kama nyenzo ya kuendeleza mfumo wa kibepari. Sheria nyingi hulenga kulinda na kuhalalisha ukandamizaji na unyonyaji wa tabaka la chini. Uchunguzi wetu umedhihirisha kuwa, mfumo wa kibepari hutumia sheria ili kumdhulumu mnyonge kama asemavyo Althusser (1981) kuwa serikali au utawala hutumia sheria ili kuendeleza na kuudhibiti utawala. Suala hili linajitokeza katika riwaya ya *Haini* kwa kuwa mahakama ilikuwa imetawaliwa na ufisadi, na mara kwa mara wanyonge walikosa kupata haki huku matajiri wakiepuka mkono wa sheria. Kwa mfano, mwanasheria mkuu alijulikana kwa sifa ya kuzisarifu na kuzifinyanga sheria za nchi ili kumfaidi na kumlinda rais wa nchi. Aidha, mwanasheria huyu anadhihirisha tabia ya kuwa kigeugeu na binafsi kwa kuwa kila mara aligeuza sheria kutegemea upande uliokuwa umetoa kiasi kikubwa cha pesa. Hili linadhihirika wakati ambapo msimulizi-mfokasi anaposema, "… zaidi ya kuwa na kipaji cha ajabu kwa kazi yake ya uanasheria, alijaaliwa pia kuwa na uhodari mkubwa wa kujigeuza mwendo na tabia ili kulinda masilahi yake. Alikuwa barakala

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1959

aliyetia fora na ubarakala aliumudu vizuri (uk. 231). Tabia hii yake ilimsaidia kuhudumu chini ya uongozi mbalimbali bila kuwa na tatizo lolote. Msimulizi-mfokasi anatueleza kuwa alikuwa ameifanyia kazi serikali ya Elizabeth wa Pili na baada ya utawala wa Kiingereza kubanduliwa alifanywa mshauri mkuu wa mambo ya kisheria wakati wa utawala wa Sultan. Baada ya wakulima na wakwezi kuuangusha utawala wa Sultani, aliaminiwa tena na serikali mpya ya Kigogo. Kwa mfano, msimulizi mfokasi anasema kuwa Kigogo hakumwona mwanasheria mwingine aliyekuwa na kipawa kama vile Chopra. Kwa hivyo, alimpachika cheo cha Mwanasheria Mkuu wa serikali yake ambapo alimwamini kuzisarifu na kuzifinyanga sheria za nchi kama alivyopenda.

Katika *Harufu ya Mapera*, watu wa tabaka la juu wanavunja sheria bila kuadhibiwa. Kwa mfano, Citizen mwanawe mwanasiasa mashuhuri Pipo Kenya anasababisha ajali barabarani, lakini hajali licha ya kuwa yeye ndiye mwenye makosa. Sababu ya tabia yake inatokana na itikadi kuwa matajiri hawafai kudhibitiwa na sheria. Citizen anamwambia mwenye gari lilogongwa kuwa, hakuna hatua ambayo ingechukuliwa na polisi hata kama wangepigiwa simu. Hili linadhihirika kupitia kwa mazungumzo kati yake na mwenye gari:

> *"Wewe kijana unajua sheria za nchi lakini? Umeligonga gari langu kutoka nyuma… ukifanya hivyo kesi inakuangukia wewe…"*
>
> *"Hapana... sina kosa, unasikia?"*
>
> *"Wacha utaona … wacha polisi waje!"*
>
> *"Ehh, ehh. Hata polisi wakija ndiyo watafanya nini?"*
>
> *"Watafanya nini?"*
>
> *"Eh, watafanya nini? Unajua babangu ni nani?"* (uk. 375).

Citizen anaposema, "Unajua babangu ni nani" anamaanisha kuwa babake ni mtu mwenye hadhi nchini ambaye hafai kudhibitiwa na sheria. Ni dhahiri kuwa ana uhakika kuwa sheria haingemwadhibu kwa kuwa babake alikuwa na uwezo wa kiuchumi ambao ulimpa fursa ya kuwahonga majaji ili kuipinda sheria. Haya yalikuja kutimia baadaye kwani hakuna hatua yoyote ya kisheria iliyochukuliwa dhidi yake, ila sheria ilibadilishwa ili kumlinda Citizen. Hali hii inamfanya Citizen kuwa na kiburi na kutojali kuhusu umuhimu wa kufuata sheria za barabarani.

Mfumo wa kibepari hautilii maanani haki kwa maskini. Kwa mfano, katika *Ndoto ya Almasi*, Almasi anafungwa kifungo cha miaka kumi bila ya hatia yoyote. Hii ni kwa sababu hakuwa na mtetezi yeyote wakati wa kesi. Kinaya ni kwamba jaji aliyemhukumu bila ushahidi, alipandishwa cheo na kufanywa jaji wa mahakama ya rufaa punde tu baada ya kesi hiyo. Almasi anashangazwa na uamuzi huu ndiposa anauliza vigezo vinavyotumiwa na serikali ili kuwapandisha watu vyeo kupitia kwa ufokasi ndani kama ilivyo katika mazungumzo haya:

> *"Kwani vigezo gani hutumika kupandisha mtu cheo katika mfumo wa mahakama?"*
>
> *"Kabila la mtu, tabia ya kujikombakomba na kutoweza kuifasiri sheria ipasavyo."*
>
> *"Hivi ni kusema sheria zetu ni sheria za mnyonge mnyongeni?"*
>
> *"Kabisa, ndiyo sababu sisi mawakili tupo kuwatetea wanyonge."* (uk. 89).

Mazungumzo ya wakili yanadhihirisha kuwa ufisadi umekuwa jambo la kawaida mahakamani, na hii ndiyo sababu haonyeshi aibu yoyote anapolijadili suala hili. Ila anaonekana kufurahia na kujivunia hali inayowakumba wananchi kwa kuwa, hali hiyo ndiyo humpa yeye kazi na kipato.

Mtindo mwingine ambao unatumiwa na mawakili na majaji kuwanyima wanyonge haki ni uahirishajiwa kesi wa mara kwa mara. Kwa kufanya hivi, watu maskini wanakosa kufuatilia kesi zao kutokana na ulimbukeni au gharama kubwa inayohusika katika shughuli za mahakama. Hali hii huwafaidi matajiri kwa kuwa aghalabu huwa wamewahonga majaji ambao hutumia mbinu hii ambayo ni ghali kwa watu wa tabaka la

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

chini. Kwa mfano, katika *Hujafa Hujaumbika*, Timazi anakosa kupata haki yake baada ya kufutwa kazi kwa misingi ya kikabila. Alipojaribu kutafuta haki, alishindwa kwa kuwa kila mara kesi yake ilikuwa ikiahirishwa hadi ilipofika wakati ambapo hakuwa na pesa za kuifutilia.

Sheria pia inatumiwa kama njia ya kuwazuia raia wanaotaka kujiimarisha kiuchumi. Katika *Nyuso za Mwanamke*, Nana anapitia vizingiti vingi wakati ambapo anataka kuanzisha biashara yake kwa lengo la kutaka kujitegemea. Mara kwa mara ananyimwa leseni ya biashara kwa kuwa wasimamizi wa idara husika wanatumia sheria kumhujumu au hata kutumia sheria hiyo kinyume ili asifanikiwe. Msimulizi-mfokasi anasimulia hali hiyo anaposema kuwa Nana alikuwa ametishwa kwa sheria ili asiweze kupigania haki yake. Kwingineko, alifitinishwa kuwa kaenda kinyume cha sheria na wadhibiti sheria na hata kunyimwa ruhusu ya kuanzisha miradi na biashara yake kupitia kwa pingu za sheria. Aidha, aliwahi kushitakiwa kipumbavu na kutiwa ndani kwa visingizio ambavyo havikuwa na ushahidi. Hali ingekuwa kinyume iwapo angekuwa bado anaishi kwa babake ambaye alikuwa tajiri na mfanyabiashara mashuhuri kwa kuwa angetumia pesa ili kupata leseni bila wasiwasi. Lakini kwa kuwa Nana alikuwa ameyaasi maisha ya kwao, mambo yalikuwa yanamwendea mrama.  Ilibidi aipitie hali ngumu kama hii ili kufahamu jinsi maisha yalivyo nje ya kasri la babake.

Katika *Makuadi wa Soko Huria*, matajiri wengi wenye ushawishi nchini na viongozi serikalini wanatumia sheria ili kuwadhulumu wananchi. Viongozi hao wanavivamia vijiji vilivyo karibu na mji, na kunyakua mashamba ya wanavijiji hivyo kwa bei rahisi. Hii ni baada ya watu wengi kutishiwa kuwa serikali ilikuwa na uwezo wa kubadilisha sheria za ardhi ili kuwafanikisha watu binafsi na wawezekaji kuyapata mashamba hayo. Hivyo basi, kutokana na wasiwasi wa kuyapoteza mashamba yao bila malipo yoyote, wanavijiji hawa walilazimika kuyauza kwa bei ya hasara. Kwa mfano, kupitia kwa ufokasi nje, msomaji anasimuliwa sehemu ya makala iliyokuwa na ujumbe huo:

> *Watu wengi pale kijijini walikuwa wakitishwa kupoteza sehemu kubwa ya ardhi zao, na bahati yao mbaya ni kwamba kijiji kilikuwa karibu mno na mji wa Songea. Hivyo, ilipotangazwa kwamba serikali ilikuwa mbioni kubadilisha sheria ya ardhi ili kuwamilikisha watu binafsi na kurahisisha wawekezaji kupata ardhi, watu matajiri na wenye uwezo kisiasa ua kimadaraka … walikuwa wakivania … vijiji na kununu…* (uk. 116).

Hali hii iliwafanikisha matajiri wachache kuyanunua mashamba kwa bei rahisi. Wengine waliokuwa na uwezo kisiasa kama vile Mheshimiwa Luhala, walitumia fursa waliyokuwa wamepewa ili kuyabinafsisha mashamba hayo. Jambo hili liliwafanya wanakijiji wengi kukosa mahali pa kufanyia kilimo chao huku matajiri wachache wakifaidika kwa kuyauza mashamba hayo kwa wawekezaji mbalimbali.

## HITIMISHO

Uchunguzi wetu umebaini kuwa kupitia kwa ufokasi ndani na nje, wahusika mbalimbali wamedhihirisha tabia, mitazamo, misimamo na hisia fulani kuhusu masuala mbalimbali kutokana na athari za itikadi zinazotawala mazingira au matamanio yao. Riwaya teule zimeonyesha kuwa itikadi za kikoloni zinazodhihirika kupitia kwa mifumo kama vile ubepari, utabaka na dhuluma bado zinatawala katika mataifa ya Afrika licha ya mataifa hayo kujipatia uhuru. Itikadi hizi zimeathiri pakubwa mitazamo na mienendo ya Waafrika ambapo wamesalia kuwa watumwa wa mataifa ya kigeni. Itikadi hizi zimedhihirika katika riwaya zote teule kama tulivyoonyesha katika uchunguzi wetu.

## MAREJELEO

Althusser, L. (1981). “Ideology and Ideological State Apparatuses”. Katika *Lenin and Other Essays*. (B. Brewster, Mtaf.). London: New Left Books.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1959

Bal, M. (1985). *Narratology. Introduction to the Theory of Narrative*. Toleo la 3 (2009). Toronto: University of Toronto Press.

Barthes, R. (1966). *Introduction to the Structural Analysis of Narratives.* Cambridge: University Press.

Chachage, S. C. (2005). *Makuadi wa Soko Huria*. Dar es Salaam: E&D Limited.

Chatman, S. (1978). *Story and Discource: Narrative Structure in Fiction and Film*. Ithaca: Cornell University Press.

Eagleton, T. (1976). *M a r x i s m and Literary Cr it ic is m*. London: Methuen.

Genette, G. (1972). *Narratology*. Imesomwa (Jumamosi 1/07/2017). http://www.signosemio.com/genette/narratology.asp

Gholami, V. (2013). "Conrad and Narrative Theory: A Narratological Reading of Selected Novels of Joseph Conrad. Tasnifu ya Uzamivu. Chuo Kikuu cha London. Haijachapishwa.

Gramsci, A. (1985). *Selections from Cultural Writings*. London: Lawrence and Wishart.

Greimas, A. J. (1973). *On Meaning*. Minnesota: University of Minnesota Press.

Hancock, B. (2002). *An Introduction to Qualitative Research.* Nottingham: Trent Focus Group.

Kagwa, F. M. (2018). *Hujafa Hujaumbika*. Nairobi: Longhorn.

Kennedy, E. (1978). *A Philosophe in the Age of Revolution: Destutt de Tracy and the Origins of 'Ideology'.* Philadelphia: American Philosophical Society.

Marx, K. (1979). *Pre-Capitalist Social Economic Formations*. Moscow: Progress Publishers.

Marx, K na F. Engels. (1977). *The German Ideology*. London: Lawrence and Wishart.

Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Tamthilia, Riwaya na Hadithi Fupi*. Nairobi: East African Education Publishers.

Mohamed, S. A. (2010). *Nyuso za Mwanamke*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Rimmon-Kenan, S. (1983), (2003). *Narrative Fiction: Contemporary Poetics*. London: Routledge.

Shafi, A. S. (2003). *Haini*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Shivji, I. (2002). Makuadi wa Soko Huria (Chachage, S. Chachage): *Hotuba ya Uzinduzi wa Kitabu, katika Mulika* Na. 26 (2000-2002): 93-97.

Todorov. T. (1990). *Genres in Discourse*. New York: Cambridge Press.

Walibora, K. (2006). *Ndoto ya* Almasi. Nairobi: Moran Publishers.

Wamitila, K. W. (2012). *Harufu ya Mapera*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.